

Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA
KAZI YA KIMISHENI ULMWENGUNI KOTE

MATESO YA KRISTO?

(Habari ifuatayo inaonyesha kusulubiwa kwa Kristo kama ilivyonukuliwa katika Mathayo 27; Marko 15; Luka 23 na Yohana 19)

Baada ya Yesu kusalitiwa, alishikwa, akafanyiwa kesi, akahukumiwa asulubiwe, akavuliwa mavazi yake, na kudungwa kwa miiba na askari wa Kirumi. Kichapo ambacho Yeye alipewa kililingana na matakwa ya sheria za Kirumi, ambapo lazima kila mtu ambaye alikuwa amehukumiwa kuuawa alikuwa hana budi kuchapwa. Lengo la kichapo hicho kilikuwa kufanya ambaye alikuwa amehukumiwa kuwa dhaifu mwilini hadi kuwa nusu mfu. Na katika kichapo hicho Warumi walitumia mkanda mfupi ambao ulishikanishwa na miiba ya ngozi, ambako mipira midogo ya miiba au vipande vya mifupa ya kondoo vyenye makali vilikuwa vimeshikanishwa. Wakati Yesu alipokuwa akipewa kichapo hicho ngozi yake ilikatika-katika na damu ikamtiririka mwilini. Vipande vyake vya nyama ya mgongoni na misuli yake ilikatikakatika ikawa kama utepe wakati ambapo mapigo hayo yalikuwa yakiendelea.

Huku wakimfanya dhihaka askari hao wakamwekea vazi nyekundu mwilini ambalo lilijaa damu yake na pia wakamweka taji la miiba kichwani. Katika Maandiko miiba huwa na maana ya dhambi, na ndiposa Mfalme wa Wafalme akawa sasa amebeba dhambi za ulimwengu mwilini mwake. Pia wakamweka



mwanzi mkononi na kumdhihaki huku wakijifanya kunyenyeka mbele zake kwa dhihaka wakisema, "Salamu, Mfalme wa Wayahudi!" Wakati Yesu akiwa na uchungu mwingi na mateso askari wakamgonga kichwani huku wakimchekelea na kumtemea mate.

Na kulingana na utamaduni ule mtaimbo

wa kuunganisha msalaba uliwekwa mgongoni mwa Kristo. Nayo mikono yake ambayo ilikuwa imenyooshwa ikafungwa kwenye mti huo ambao ulikuwa na takriban ratili 75 hadi 125. Yesu akapelekwa hadi Golgotha kuuawa huko, na huku akiwa mdhaifu alipepesuka polepole kutokana na uzito aliokuwa amewekewa na ikawa vigumu Yeye kuendelea na safari hiyo. Hapo ndipo mtu mmoja ajulikanaye kama Simoni akasaidia kubeba msalaba huo.

Hapo saa tatu (katika lisaa la tatu) mwendo wa asubuhi Yesu akatupwa chini sakafuni na viganja vya mikono yake vikapigiliwa miiba ya chuma. Halafu ishara ikawekwa pale kwenye msalaba likiwa na tangazo liliosema: "Huyu ni Yesu, Mfalme wa Wayahudi." Msalaba nao ukanyanyuliwa na akawekewa miiba ya chuma miguuni mwake ili kushikanisha miguu yake na mbao ya msalaba.

Kusulubisha ilikuwa ni njia moja ya kutekeleza hukumu ya kifo lakini ni njia ambayo ilikuwa na uchungu mwingi na aibu kubwa. Njia hiyo ya kumwadhibu mtu

(Inaendelea kutoka ukurasa 2)

MAMBO AMBAYO

BIBLIA

Inafundisha Kuhusu...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,

Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,

I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa I)

ilikuwa hasa ikitekelezwa dhidi ya watumwa, wageni, wasaliti, na wahalifu wabaya sana. Lengo lake lilikuwa kufanya aliye hukumiwa kifo kuwa na uchungu na mateso ya hali ya juu. Hapo basi wahalifu wawili wakasulubiwa pamoja na Yesu na kuangikwa kwenye misalaba kando yake.

Huku akiwa hapo msalabani na akiona uchungu mwangi Yesu alipata mateso ya kimwili na ya kiakili. Akawatazama umati uliokuwa umekusanyika hapo na kuomba, "Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo." Hata ingawa Yesu alikuwa na nguvu za kuita malaika ili wamwokoe Yeye alikuwa amejitoa ili awe mwanakondoo wa sadaka kwa sababu aliwapenda wanadamu. Na hapo saa sita mchana (lisaa la sita) akalia kwa sauti kubwa, "Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu." Wakati huo Yesu akifa ndipo pazia la hekalu lilikatika pande mbili kutoka juu hadi chini; pia kukawa na mtetemeko wa ardhi. Kutoka sasa watu wote wangeweza kumfikia Mungu kuitia kwa damu ya mwana wake.

Yesu akateseka na kuvumilia kifo chenye uchungu mwangi ili ulimwengu uokoke kwa sababu ya sadaka ya mwili wake. Naye askari mmoja alipoona Kristo amekufa akamzunga mkuki upande wa mbavu zake na ndani mwake kukatoka damu na maji. Hapo Shetani akafikiria kwamba ameshinda kwa sababu sasa Masihi wa Mungu ameshakufa . . . lakini Jumapili ikaingia! Yesu akafufuka kuoka kwa wafu kwa ushindi mkuu na sasa yu hai milele na milele!

—mws

UKWELI WA INJILI

Gazeti la 'Ukweli wa Injili' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambaa umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi ktuokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambaa hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinasi na wa upendo ambaa msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

UAGIZAJI

Ukweli wa Injili ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongoza. Tute mbelee katika mtandao wetu wa www.thegospeltruth.org ili uagize kuitia kwa orodha yetu ya anwani pepe ili upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambaa wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

WASILIANA NASI

Gazeti la Ukweli wa Injili linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimisheni ambazo sisi hutenda huwezesha kuitia kwa matolea ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lo lote likawaharibu
—Kutoka 12:13

Asante Mungu kwa hiyo damu! Malaika wa kifo alipoona damu imepakwa kwenye miimo ya milango ya wana wa Israeli walipokuwa Misri alipita juu yao. Na wakati tutakaposimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu ataona damu ya mwana wake na hapo tutaokolewa kutokana na kifo cha milele.

Kuna nguvu katika damu ya Yesu za kutuhoa kutoka kwa shimo la dhambi ambalo lina kina kikubwa. Wakati mtu ameshikwa na nguvu za mwili inaonekana kama kwamba hakuna njia yoyote ya yeze kuweza kuishi maisha matakatifu, lakini hapo tunasau kwamba damu ya Yesu inao uwezo wa kumtakasa mwenye dhambi aliyetokomea dhambini. Hata ingawa Yesu hapo karibu miaka 2000 iliyopita, damu yake bado hiyo ingali haijapoteza nguvu zake.

Katika robo hii ya mwaka tunakamilisha masomo yetu kuhusu kanuni za kanisa kwa kujifunza kuhusu meza ya Bwana. Katika Agano la Kale wanyama ndio walitolewa kama sadaka kwa ajili ya utakaso wa dhambi: "Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi" (Waerania 10:4). Kristo alijitoa kwa Mungu kama sadaka kamili na kupitia kwa umwagikaji wa damu kuna nguvu za kumpatia mwanadamu uhuru kutokana na dhambi. Mimi ninakumbuka wakati mwingi nikubujikwa na machozi wakati nikishiriki meza ya Bwana nilipokuwa nikiwaza kuhusu sadaka kuu ambayo Yesu alitoa. Upendo wake ni mkuu na Yeye alilipa gharama ya hali ya juu kabisa kwa ajili ya wokovu wetu.

Ulimwengu wetu unatilia umuhimu sikuu ya Krisimasi na wengi husherehekeza kuzaliwa kwa Kristo wakati huo wa Disemba. Lakini tunahitaji kuzingatia kwamba Kristo hakuzaliwa katika mwezi wa Disemba na wala hakutoa maagizo yoyote kwamba kuzaliwa kwake kusherehekewe. Lakini Yeye aliamuru kwamba watu wake wakumbuke kifo chake kupitia kwa sherehe ya meza ya Bwana. Hata ingawa Biblia haina mwongozo wowote wa ni lini meza ya Bwana inastahili kusherehekewe, ni jambo bora ikiwa makusanyiko ya mahali pamoja watakuwa na ushirika huo wa meza ya Bwana Jumapili ya wiki ambayo Yesu alififuka.

Utamaduni wa Kikristo na mifano yake ni mambo muhimu katika ibada hiyo ya meza ya Bwana. Mimi najua watu wengi hawapendi kushiriki pamoja kutoka kwa kikombe kimoja, badala yake wanapenda kila mtu awe na kikombe chake. Lakini mimi sijawahi kusikia kwamba mtu amekuwa mngonjwa kwa kushiriki kutoka kwa kikombe kimoja cha ushirika. Mimi mwenyewe nishawahi kushiriki kikombe hicho katika vikundi vyta watu ambako walikuwa na magonjwa tofauti lakini kamwe sikuwahi kuwa mngonjwa kutokana na ushirika huo wa kikombe kimoja.

Maji ya mizabibu ndio yalitumika katika nyakati za Biblia kwa matumizi ya meza ya Bwana. Hata ingawa maji hayo ndio bora kabisa kutumiwa kwa sababu ya umuhimu wake mimi nishawahi kuwa mahali ambako hakukuwa na mizabibu. Badala ya kuhepa kufanya meza ya Bwana kwa sababu ya ukosefu wa matunda ya mizabibu sisi tulitumia aina tofauti za vinywaji. Katika mahali moja tulichanganya soda nyeusi na juisi nyingine ya kienyeji. Ninaamini kwamba Mungu alipendezwa na sisi kusherehekeza meza ya Bwana kwa njia hiyo.

Ni baraka kubwa kwetu kushiriki katika mateso ya Bwana wetu: "Ee Bwana, sisi twashiriki katika mateso yako..."

Michael W. Smith

Aprili 2015





Viungo vya Mkate Usiotiwa Chachu

Ni rahisi sana kutengeza mkate usiotiwa chachu. Viungo vyake ni unga na maji.

Viungo vyenyewe:

Kikombe kimoja au kikombe kimoja na nusu cha unga ngano asilia.

Kikombe kimoja cha maji

Weka ngano kwenye bakuli. Kwa utaratibu ongeza maji kwa ngano hiyo huku ukikoroga hadi doneg la unga liwe laini. Endelea kuungeza maji au ngano hadi wakati ambapo doneg hilo litakapokuwa nzito hivi kwamba unawenza kuunda mkate amba ni tambarare na wenye mviringo kwa kutumia mikono yako ambayo umeipaka mafuta.

Weka mkate huo kwenye kibati cha kuoea kilicho na mafuta. Pika kwa kipimo cha moto cha Fahrenhaiti 350 kwa dakika 15 hivi.

Matokeo yake ni: Mkate mmoja.



“Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.”

I Wakorintho 11:24

MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

SOMO: KANUNI YA MEZA YA BWANA

Somo la Biblia: Basi, ikiwa mimi niliye Bwana na Mwalimu nimewaosha nyinyi miguu, nanyi pia mnapaswa kuoshana miguu. –1 Wakorintho 11:26

Muhstasari: Meza ya Bwana ni kanuni ya Biblia ambayo ilianzishwa kama ukumbusho wa mateso na kifo cha Yesu Kristo ambaye mwili wake ulivunjika na akamwaga damu yake kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu.

Soma: Mathayo 26:17-30; 1 Wakorintho 11:20-34 (Tazama pia: Luka 22:7-22; Marko 14:12-26).

I. Ilianzishwa Wakati wa Pasaka

- A. Kutoka 12:12-15 Pasaka ya huko Mistri.
- B. Mathayo 26:17-20 Pasaka ya mkate usiotiwa chachu.
- C. Luka 22:7-16 Pasaka inaandaliwa.

II. Ilianzishwa na Kristo

- A. Mathayo 26:26-29 Yesu anawapatia wanafunzi wake ushirika wa meza ya Bwana.
- B. 1 Wakorintho 11:23 Kama nilivyopokea kutoka kwa Bwana.

III. Kusudi la Ushirika wa Meza ya Bwana

- A. Ukumbusho wa Agano Jipyä
- B. 1 Wakorintho 11:24b,25b “Kwa ajili ya kunikumbuka”
- C. 1 Wakorintho 5:6-8 Kuonyesha kifo cha Bwana.

IV. Mifano ya Mkate

- A. Mathayo 26:26 Mwili wa Kristo.
- B. 1 Wakorintho 11:24 Mwili wa Kristo amba ulivunjika.
- C. 1 Wakorintho 10:17 Kanisa—mwili wa Kristo.
- D. 1 Wakorintho 5:6-8 Mkate amba hujatiwa chachu.

V. Mifano ya Uzao wa Mizabibu

- A. Mathayo 26:28-29 Damu ya Yesu iliyomwagika.
- B. 1 Wakorintho 10:16 Ushirika wa damu.
- C. 1 Wakorintho 12:13 Kunywa kutoka kwa yule Roho mmoja.

VI. Njia Inayofaa ya Kufanya Ushirika wa Meza ya Bwana

- A. Marko 14:22 Yesu akachukua mkate, akaubariki, akaumega, halafu akawapatia.
- B. Marko 14:23 Yesu akachukua kikombe, akashukuru, akawapa, na wote wakanya kutoka kwa kikombe hicho.
- C. Tazama pia: 1 Wakorintho 11:23-26.

VII. Kutamatisha Meza ya Bwana

- A. Mathayo 26:30 Wakaimba wimbo.
- B. Marko 14:26 Wakaimba na kuondoka.

VIII. Ushirika Unatumiwa Vibaya huko Korintho

- 1 Wakorintho 11:20-22, 34: Ushirika huo wa Wakristo wa Korintho ulitilia mkazo watu kula kwa kimwili badala ya kuwa na maana halisi ya ushirika wa meza ya Bwana, ambayo ni ukumbusho.

IX. Kanuni kwa Waumini

- A. 1 Wakorintho 11:27-28 Jichunguzeni.
- B. 1 Wakorintho 11:29-32 Matokeo yake.

X. Kanuni Ambayo Ilihitaji Kudumishwa na Kanisa

- A. Mathayo 28:20 Kuyashika yote.
- B. 1 Wakorintho 11:2 Dumisheni kanuni zote.
- C. 1 Wakorintho 11:25 Fanyeni hayo.

Tamati:

Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe

– 1 Wakorintho 11:28

KANUNI YA MEZA YA BWANA

Nakala ya kuandamana na mafunzo ya Biblia

PASAKA KATIKA AGANO LA KALE

Karibu mika 3500 Musa na wana wa Israeli walikuwa wamekaribia siku ya kutoka utumwani Misri. Mungu naye akawaambia watu hao wake kutoa sadaka ya mwanakondoo asiye na ile na kuweka damu yake kwenye miimo ya milango. Usiku huo malaika wa kifo akapita juu ya nchi ya Misri kuua kila mwana mzaliwa wa kwanza katika kila nyumba. Lakini kukawa na wokovu kutoka kwa kifo katika nyumba zote ambako damu ya mwanakondoo ilikuwa imepakwa.

Basi hapo pasaka ikaanzishwa ili kila mwaka kuweko na ukumbusho wa wokovu wa kihistoria na wa ajabu (Kutoka 12:12-15).

YESU ALIANZISHA KANUNI YA USHIRIKA WA MEZA YA BWANA

Baada ya mika 1500 hivi Yesu alikaa na wanafunzi wake kushiriki nao chakula cha Pasaka (Luka 22:7-16). Yeye alijua kwamba baada ya masaa machache angesulubiwa kama sadaka ya mwanakondoo kwa ajili ya dhambi ya wanadamu. Basi akachukua mkate usiotiwa chachu na kikombe cha tunda la uzao wa mzabibu na kufanya ushirika wake wa kwanza wa meza ya Bwana (Mathayo 26:26-29). Basi kanuni hiyo ilianzishwa na Kristo na kuhakikiwa na mtume Paulo; "Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi . ." (1 Wakorintho 11:23).

Yesu akaanzisha kumbukumbu la Agano Jipyä ambalo lilifanana na Pasaka ya Agano la Kale. Wanadamu wanaokolewa kutokana na kifo cha milele kupitia kwa damu ya mwanakondoo Yesu Kristo. Yesu naye akawaagiza wanafunzi wake kufanya ushirika huo; "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" (1 Wakorintho 11:24b). Meza ya Bwana ambayo inafanywa na kanisa ni ibada ya ukumbusho ili watu wa Mungu wasiwhi kusahau uchungu na mateso ambayo Mwokozi wao alipitia: "Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwitangaza mauti ya Bwana hata ajapo" (1 Wakorintho 11:26).

MKATE UNAWAKILISHA MWILI WA KRISTO

Meza ya Bwana ni moja ya kanuni ambazo zinapatikana katika

Agano Jipyä. Kanuni hii inaashiria mambo makuu wakati ambapo ibada hii ya ushirika inafanywa. Yesu alitumia mkate usiotiwa chachu (wakati na Pasaka) na akasema, "Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu . ." (1 Wakorintho 11:24). Yeye alipigiliwa misumari hapo msalabani na akadungwa mkuki. Mwili wake ulivunjavunjwa ili tupate kuokolewa. Mkate nao ni mfano wa mwili uliosulubiwa. Hata ule mkate usiotiwa chachu (kwenye maandiko) ni mfano wa mwili wa Kristo, yaani Kanisa la Mungu:

"Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisitulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja" (1 Wakorintho 10:17). Kama ulivyo mkate usiotiwa chachu, na kama jinsi mkate huo ulivyoshikamana pamoja kwa njia ya mbengu nydingi za ngano kuja pamoja kuunda mkate huo mmoja, ndivyo liliyvo kanisa la Kristo. Kanisani humo watu wenye maumbile tofauti na historia tofauti

huunganishwa pamoja kwa njia ya umoja wa mwili wake, wakati ambapo wanabadilishwa kwa wokovu ambaa huatikana kwa nguvu za Kristo.

JUISI YA MZABIBU INAWAKILISHA DAMU NA MATESO YA KRISTO

Juisi ambayo Yesu alitumia ilitokana na matunda ya msabibu. Hii iliwakilisha damu ya Kristo ambayo ilimwagwa msalabani (Mathayo 26:28). Matunda hayo ya mzabibu hayana budi kufinyangwa ili kupata maji yake. Kristo alipigwa viboko, akachapwa, halafu akasulubiwa ili kupitia damu yake tuweze kupokea msamaha wa dhambi. Kila mtoto wa Mungu ana ushirika kupitia kwa damu ya Kristo (1 Wakorintho 10:16).

NJIA INAYOFAA YA KUFANYA USHIRIKA WA MEZA YA BWANA

Kuna njia njia nydingi ambazo makanisa hutumia kusherehekea ushirika wa meza ya Bwana. Ni jambo muhimu Wakristo wasipoteze ile maana ya ushirika huo wanapofanya sherehe

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)



FANYENI HIVI
KWA
UKUMBUSHO
WANGU.

(Endelea kutoka ukurasa 5)

hizo. Yesu alichukua mkate huo ambao haukutiwa chachu. Akaubariki na kuumega halafu akawapatia wanafunzi wake (Marko 14:22). Hii ndio njia inayofaa na ya kibibilia ya kufanya meza ya Bwana. Makanisa mengi hutumia biskiti nyembamba iliyo kama karatasi lakini ambayo hufanya maana ya kuvunjika vunjika kwa mkate kupotea. Halafu Yesu “Akatwaa kikombe, akashukuru, akawapa; wakakinywea wote” (Marko 14:23). Walikunywa kutoka kikombe kimoja. Jambo hili halipendezi kimwili lakini lilikuwa kitendo cha mfano chenye maana kubwa ya kiroho. Watu wa Mungu walinywea kutoka kwa kikombe cha mateso ya Bwana wetu. Huu ndio ushirika wa kweli, na ndio maana ya ushirika. Hapo mwishoni mwa ushirika huo wanafunzi waliimba wimbo na kuondoka (Marko 14:26). Kunakuweko baraka maalum wakati Wakristo wanapofuata tamaduni na kuondoka mezani mwa Bwana kwa njia ambayo inafanana na sherehe ya wanafunzi hao wa kwanza. Hatustahili kupotosha au kubadilisha mfano huo wa Biblia.

MATUMIZI MABAYA YA KANUNI YA MEZA YA BWANA

Wakristo wa Korintho hawakuzingatia meza ya Bwana kwa njia inayofaa. Ndiposa mtume Paulo akawakemea na kuwapa maagizo (1 Wakorintho 11:20-24, 34). Kusanyiko hili lilikuwa likifanya maadhisho ya meza ya Bwana kuwa wakati na sherehe ya kula kwa pupa. Wao walikuwa wamepoteza sifa kamili ya kanuni hiyo. Ndiposa Mtume Paulo akawaagiza wale nyumbani mwao na kwamba meza ya Bwana haikuwa wakati bora wa wao kujaza tumbo zao. Huu ultakiwa kuwa wakati wa kumkumbuka Kristo kwa njia ya sherehe hiyo yenye maana kubwa.

USHIRIKA WA WAUMINI

Meza ya Bwana ni kanuni ambayo inastahili kufuatwa na watu waliokoka (1 Wakorintho 11:27-32). Paulo alisema kwamba yejote anayekula mkate au kunywa kutoka kile kikombe kwa njia isiyostahili atakuwa na hatia dhidi ya mwili na damu ya Bwana. Kila mtu basi anahitaji kujichunguza kabla ya kuwa mshirika; kanisa halina wajibu wa kumchunguza mtu. Huu ni wakati wa kila mtu kujichunguza kindani, jambo ambalo ni zaidi ya mtu kudai kwamba yeje ni mwokovu. Huu ni wakati wa mtu kuchunguza maisha yake, tabia yake, kazi anazofanya, na mielekeo ya maisha yake n.k. Wengi wa washirika wa Korintho

walikuwa wagonjwa, wanyonge na hata wengine walikuwa wamekufa kwa sababu ya ukosefu wa kuwa na maana ya kiroho wakati wakishiriki meza ya Bwana. Makosa haya hayakumaanisha kwamba mtu angetenganishwa milele na Mungu, lakini ni jambo lililomchokoza Mungu na kuleta hukumu. Bwana alikuwa akiwapatia nidhamu ili wasihukumiwe katika maisha yao ya milele kama ulimwengu



“Ni ombi letu kwamba kanisa la Mungu litakuwa na uaminifu wa kusherehekeea . . . meza ya Bwana hadi hapo wakati atakaporudi.”

utakavyohukumiwa (1 Wakorintho 11:29, 32). Meza ya Bwana ni jambo lenye uzito mkubwa na kila mtu anahitaji kuishiriki kwa uangulari na kwa kumwabudu Mungu.

KILA KIZAZI KINASTAHILI KUADHIMISHA MEZA YA BWANA

Ushirika wa meza ya Bwana ni jambo lililokweko hata wakati wa mitume na kila kizazi kinatakiwa kiufuate. Yesu alifundisha kanisa lake “kuyashika yote niliyowaamuru ninyi” (Mathayo 28:20). Naye Mtume Paulo aliambia makanisa “nanyi mmeyashika yale mapokeo vile vile kama nilivyowatolea” (1 Wakorintho 11:2). Yesu naye akasema “fanyeni hivi” (1 Wakorintho 11:25). Ni ombi letu kwamba kanisa la Mungu litakuwa na uaminifu wa kusherehekeea sadaka ya Kristo kwa kusherehekeea meza ya Bwana hadi hapo wakati atakaporudi.

—mws

MASWALI na MAJIBU

Je, tunastahili kuwa na sherehe ya Meza ya Bwana baada ya muda upi?

KWA NJIA YA WAZI KABISA KANISA LIMEAMRIWA KUSHEREHEKEA MEZA YA BWANA. WATU AMBAO HAWAKO TAYARI KUSHIRIKI MEZA YA BWANA WANA MAHITAJI YA KIROHO AMBAYO WANASTAHILI KUMPELEKEA BWANA.

Yesu hakuambia kanisa linatakiwa kuwa na meza ya Bwana baada ya muda gani. Badala yake maneno aliyosema yalikuwa "Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki . . ."

(1 Wakorintho 11:26). Swala la ni mara ngapi meza ya Bwana inatakiwa kufanywa ni jambo ambalo linaachiwa kila mshirika na kila ushirika kuamua. Lakini ni muhimu kuzingatia kwamba kupitia kwa kanuni hii Kristo alikuwa akifuata mfano wa Pasaka ya Waisraeli ambayo ilisherehekewa mara moja kila mwaka.

Kuna wale ambao huwa na ushirika wa meza ya Bwana mara moja au zaidi kila wiki. Hata ingawa jambo hilo si mbaya, lakini kwa njia moja au nyingine kuna hatari kwamba ushirika huo unaweza kufanywa uwe wa kuchukuliwa kijuujuu na kuufanya kuwa jambo la mazoea tu. Halafu pia kuna hatari kwamba kuna watu ambao watajihisi wako salama kwa sababu ya kushiriki meza ya Bwana mara nyingi. Lakini mtu kamwe hapati wokovu kutokana na kushiriki katika kanuni hiyo ya meza ya Bwana. Mtu hupata wokovu

kwa njia ya neema kupitia kwa imani ambayo hufanya mtu kuishi maisha matakatifu.

Je, watoto wanastahili kushiriki meza ya Bwana?

MAANDIKO HAYAJAPEANA UMRI AMBAO WAHSIKA WANASTAHILI KUFIKISHA ILI WASHIRIKA MEZA YA BWANA LAKINI YANATOA MASHARTI

FULANI. Kwa njia ambayo ni wazi kabisa Maandiko yanasema "Lakini mtu ajihoji mwenyewe" (1 Wakorintho 11:28). Watu wale ambao wanastahili kushiriki meza ya Bwana ni wale ambao wameokoka. Mtoto mchanga au mtoto wa miaka miwili hana uwezo wa kuijhoji mwenyewe. Kama vile kumbatiza mtoto mchanga ni jambo lililo kinyume na Maandiko, ndivyo ilivyo kwa mtoto mchanga kushiriki meza ya Bwana. Ni wajibu wa mzazi kujua mtoto wake na kupanga wakati ambapo mtoto huyo ataanza kushiriki meza ya Bwana. Ilhali wazazi wanahitaji kuwalea watoto kwa njia ya kiungu, ushirika wa meza ya Bwana ni kumbukumbu maalum ambayo imetegewa wale ambao wamezaliwa mara ya pili. Watoto wanastahili kutambua maana kubwa ya Wakristo kushiriki meza ya Bwana na kwa hivyo waheshimu ibada hiyo. Ikiwa mtoto atashiriki meza ya Bwana anastahili kuwa na ujuzi wa kibinagsi wa wokovu.

Je, tuseme nini kuhusu kubadilishwa kwa viungo?

KUBADILISHWA KWA VIUNGO NI MOJA YA THIOLOJIA ZA UWONGO KUHUSIANA NA SIFA YA MKATE WA USHIRIKA WA MEZA YA BWANA NA UZAO WA MZABIBU.

Fundisho hili ambalo linafundishwa na kanisa la Katoliki (kanisa la Kirumi) linasema kwamba wakati wa sherehe za meza ya Bwana sifa za "mkate na mvinyo" zinabadilika zinakuwa mwili na damu

ya Kristo, hata ingawa zinaendelea kuonekana kubaki vile vile. Mafundisho hayo yanatokana na yale maandiko ambako Yesu alisema "huu ndio mwili wangu" na "hii ndiyo damu yangu" (Mathayo 26:26, 28). Lakini Yesu hakuwa akimaanisha hayo kwa njia ya moja kwa moja, kwa sababu damu yake ilikuwa ingali ndani yake na kwa kweli alikuwa angali mwilini mwake. Yeye alikuwa akisema kwa njia ya mfano. Alikuwa akinena kwa njia ya kulinganisha. Lakini pia alisema kwa njia ya moja kwa moja katika 1 Wakorintho 11:26 "Maana kila mwulapo mkate huu . . ." Akawaambia wanafunzi wake wawe wakishiriki meza ya Bwana "kwa ukumbusho wangu" (Luka 22:19). Hii ni kumaanisha kwamba Yeye mwenyewe hakuwa ndani ya mkate wa ushirika. Mkate na tunda la mzabibu ni mifano tu ya mwili na damu ya Kristo.

—mws





JE, WAJUA?

Nao walipokwisha kuimba walitoka kwenda mlima wa Mizeituni

—Marko 14:26.

Wayahudi walisherehekeea Pasaka kwa kuimba wimbo wa Hallel ama Halleluyah. Wimbo huu umenukuliwa kutoka Zaburi 113-118, Zaburi ambazo hutumika kwa sifa na kwa kutoa shukrani kwa Mungu. Mara nyangi Zaburi 113-114 ziliimbwa kabla ya chakula kuliwa na Zaburi 115-118 kuimbwa baada ya chakula kuliwa.

Bila shaka hizo ndizo nyimbo ambazo Yesu na wanafunzi wake waliimba kabla ya kuondoka kwenda mlima wa Mizeituni.



Kushiriki Mateso Yake

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA
Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara.... ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake. —Wafilipi 3:8-10

Mtume Paulo alihesabu kila kitu maishani kuwa ni hasara ili yeye aweze kujua maisha na nguvu za Kristo kwa njia kamilifu. Inasemekana kwamba mtume Paulo alikatwa kichwa kutokana na imani hiyo yake kwa Kristo. Na kulingana na maandishi ambayo mtume Paulo aliandika mimi nina imani kwamba mtume huyo alikaribisha kifo hicho kama vile alivyokaribisha mambo mengine masumbufo maishani mwake.

Bwana Yesu aliacha utukufu wote wa Mbinguni na kuja ulimwengu ulio na dhambi ili kuweza kuwa na ujuzi wa maisha haya na akajitoa kama sadaka kwa ajili ya dhambi yetu. Kwa kweli sisi tuna deni la Yesu ambalo kamwe hatuwezi kulipa kutokana na kipawa alichotupatia cha wokovu na cha maisha ya milele. Ni heshima kuu na baraka kuu sisi tukinywa kutokana na kikombe cha mateso ya Kristo.

Mmoja wa msomi wa kwanza wa Kikristo ambaye aliiwa Origeni alisema kwamba mtume Petro alihisi kwamba haikuwa haki yeye kuuawa kwa njia moja na Bwana wake, na kwa hivyo akasulubiwa huku kichwa chake kikiwa ndicho kilicho kwenye upande wa chini. Hili jambo lilingana na matakwa yake.

Mateso yetu kamwe haiwezi kulinganishwa na yale ya Kristo. Yeye alikataliwa, akasalitiwa, akakanwa, akasemwa uongo, akaambiwa amesema yale ambayo hakusema, akatemewa mate, akapigwa mijeledi, na hata akasulubiwa. Basi wewe mtoto wa Mungu usikate tamaa na usife moyo wakati wa mateso na majoribu: “Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe” (1 Petro 4:13).

